*Hekima, Umoja, Amani, Ni ngao Zetu!*

# NCHI YETU

**Tanzania imara, Kazi lendelee**

www.maelezo.go.tz Toleo la 239 | 08 Juni 2022 | Idara ya Habari MAELEZO | TANZANIA




HALIUZWI

# TAHARIRI

## Vyombo vya Habari na Jukumu la Kuelimisha Wananchi Kuhusu Sensa ya Watu na Makazi

Vyombo vya Habari hapa nchini vina dhima ya kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu, ili wananchi waweze kuelewa lengo na faida ya sensa hiyo kwao binafsi na Taifa kwa ujumla.

Kwa muktadha huo, navipongeza vyombo vya habari kwanza kwa kazi viliyoanza kufanya kwa uzalendo usio kifani katika kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka huu.

Hivi karibuni, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bw. Mohammed Abdulla alitoa rai Mei 27, 2022 katika mkutano wa wamiliki wa vyombo vya habari kushiriki kikamilifu katika kuendelea na kazi ya kuwaelimisha wananchi kuhusu maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Kwa muktadha huo, Idara ya Habari (MAELEZO) kushirikiana na ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Wamiliki wa Vyombo vya Habari wanayo dhima ya kutoa elimu ya sensa kwa Watanzania ili waweze kutoa taarifa sahihi wakati wa kuhesabiwa.

Aidha, vyombo hivyo vitoe elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa sahihi wakati wa sensa, kwani utoaji wa taarifa sahihi ni jambo muhimu katika sensa, kupatikana kwa taarifa sahihi kutaiwezesha Serikali kupanga mipango, na Sera sahihi katika kuwahudumia wananchi ili waweze kufikia maendeleo endelevu.

Pia, takwimu sahihi zitaiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi ambayo yataakisi hali halisi ya wananchi wake na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo.

Katika hili kila chombo kinaombwa walau kipindi kimoja kwa wiki kinachozungumzia sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 pamoja na masuala muhimu yatakayomfanya mwananchi kujiamini na kushiriki vyema katika sensa hiyo.

Kwa nyakati tofauti, Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Mhe. Anne Makinda amevipongeza vyombo vya habari kwa namna vinavyoshiriki kutoa elimu ya sensa kwa wananchi kupitia vipindi mbalimbali vya redio, televisheni, mitandao ya kijamii pamoja na habari na makala kupitia magazeti mbalimbali.

Mkutano huo, ulifanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere, Jijini Dar es Salaam ukiwashirikisha wamiliki wa vituo vya Televisheni, Redio, Magazeeti na Mitandao ya Kijamii.



# Magufuli Alinifundisha Mambo Mengi – Rais Samia

**Na Lilian Lundo - MAELEZO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amesema Hayati John Pombe Magufuli amemfundisha mambo mengi alipokuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Rais Samia amesema hayo leo, Juni 8, 2022 aliposimama kuwasalimia wananchi wa Bwanga wilayani Chato, mkoani Geita akiwa safarini kuelekea mkoani Kagera.

"Awamu iliyopita nilikuwa Makamu wa Rais chini ya kaka yangu marehemu John Pombe Magufuli, alinifundisha mambo mengi sana, niliisoma dhamira yake vizuri sana jinsi ya kupeleka nchi hii," alisema Rais Samia.

Rais Samia amewahakikishia Watanzania kwamba, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita ambapo miradi yote iliyoanza kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita na hakutakuwa na mradi ambao utakufa au hautaendelezwa.

Aidha, amesema kuwa, miradi ya zamani itatekelezwa sambamba na miradi mipya inayokuja kwa dhamira ileile ya kuleta maendeleo kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

"Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na yeyote anayekaa kuongoza Serikali, lengo ni kuhudumia Wananchi na kupeleka maendeleo kwa Wananchi na tutafanya hivyo jinsi hali ya uchumi itakavyoruhusu," alisema Rais Samia.



# Serikali Yatoa Bilioni 100 Kupunguza Bei ya Mafuta

**Na Mwandishi Wetu – MAELEZO**

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 100 kupunguza makali ya bei ya mafuta nchini.

Akizungumza na wakazi wa Wilaya ya Chato katika eneo la Bwanga, Mkuu wa Nchi amesema Serikali itaendelea kutoa ruzuku hiyo mpaka bei za mafuta duniani zitakapokaa sawa.

"Bei ya mafuta duniani imepanda kutokana na nchi za Urusi na Ukraine ambazo ziko kwenye vita, na nchi mojawapo inazalisha gesi, sasa gesi haitoki kwenye nchi hiyo kutokana na vita, hivyo dunia nzima imehamia kwenye mafuta ambayo sisi tulikuwa tunanunua.

"Mahitaji ya mafuta yamekuwa makubwa kutokana na nchi nyingi kuyatumia, hivyo bei zimepanda, hili sio suala la Tanzania pekee bali ni dunia nzima," ameeleza Mheshimiwa Rais.



# Mwananchi Hatokufa kwa Shida – Rais Samia

**Na Ahmed Sagaff – MAELEZO**

Rais Samia Suluhu Hassan amesema Serikali anayoiongoza itaendelea kutatua shida mbalimbali za wananchi kama ilivyoahidi katika Ilani ya Chama kilichopo madarakani.

Mkuu wa Nchi ameyasema hayo leo wakati akiwasalimia wananchi wa Wilaya ya Muleba mkoani Kagera katika ziara yake ya kikazi katika mkoa huo.

"Hatutakufa kwa shida, kwa serikali hii mwananchi hatakufa kwa shida, tutakufa kwa uzee na maradhi lakini sio kwa shida," ameeleza Rais Samia.

Katika ziara hiyo, Rais Samia ameambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso, Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Hamad Masauni pamoja na mawaziri wengine.




# Simamieni Matumizi ya Fedha za Wananchi – Rais Samia

**Na Ahmed Sagaff – MAELEZO**

Rais Samia Suluhu Hassan amewataka viongozi wa Mkoa wa Kagera kusimamia fedha za wananchi ili zitumike katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye halmashauri za mkoa huo.

Mkuu wa Nchi ametoa maelekezo hayo katika Wilaya ya Biharamulo aliposimama na kuzungumza na wananchi wa wilaya hiyo akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo.

Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi tunaendelea na sera ile ile ya kupeleka maendeleo kwa wananchi, na jinsi wananchi mnavyojituma tukikusanya nyingi tutaleta nyingi kwasababu sisi hatuna faida ya kukaa nazo kule na kuziona zinatuna kwenye mifuko kule.

“Zikituna kwenye mifuko tunazirusha tunazirudisha kwenu wananchi, na kwa maneno ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Mbunge, fedha nyingi sana zimeletwa kwa wananchi huku.

“Niwaombe sana wale walioaminiwa kwenye Halmashauri kuzitumia fedha zile vyema ili yale tuliyoyakusudia kwa wananchi yapatikane, niwaombe sana Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na RAS simamieni matumizi ya fedha za wananchi mkisaidiana na wabunge wa maeneo,” ameeleza Mheshimiwa Rais.



# Mnada wa Kahawa Kufanyika kwa Uwazi

**Na Ahmed Sagaff – MAELEZO**

Serikali imewaelekeza wanunuzi wa kahawa ya robusta inayotarajiwa kuuzwa kwa mnada wiki ijayo wahakikishe hawanunui chini ya shilingi 1,650 kwa kilo huku akieleza kuwa kahawa ya arabika iliuzwa jana kwa shilingi 3,720 bila makato.

Akizungumza katika Wilaya ya Biharamulo leo, Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe amesema bei hizo zimetokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yanayolenga kuinua hali za wakulima nchini.

"Hawawezi kutupiga bao kwasababu tunaijua bei ya dunia, kwahiyo muda wa kuibiana na wakulima umepitwa na wakati, na mfumo wa mnada ni wa wazi.

"Tutaweka TV minadani mwananchi unaangalia ukiona bei hailipi una haki ya kukataa na kusema siuzi kahawa yangu kwasababu hakuna mtu aliyekusaidia kwenda kulima," ameeleza Waziri Bashe.



# Serikali Haitawaangusha – Rais Samia

Na Ahmed Sagaff - MAELEZO

Rais Samia Suluhu Hassan amewaahidi wakazi wa Wilaya ya Muleba kuwa Serikali anayoiongoza itaendelea kufanya kazi zaidi ili kutatua kero zinazowakabili.

Mkuu wa Nchi ameyasema hayo leo katika eneo la Izigo wilayani Muleba mkoani Kagera aliposimamisha msafara wake na kuzungumza na mamia ya wananchi waliojitokeza kumpokea.

"Najua kwamba wananchi wa Muleba mna matumaini makubwa na Serikali yenu, nataka niwaambie kuwa Serikali haitawaangusha, Serikali ya CCM tunakwenda kufanya kazi zaidi ili kuhakikisha kero zote zinazowakabili zinaondoka," ameeleza Mheshimiwa Rais.

Pamoja na hayo, Rais Samia amesema Serikali itahakikisha inamaliza kero zote katika sekta zote ikiwamo elimu, afya, maji na umeme.



# Rais Samia Awahakikishia Watanzania Neema

**Na John Mvungi- MAELEZO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewahakikishia Watanzania kuwa Serikali ya Awatmu ya Sita inaendeleza miradi yote iliyoanzishwa katika Awamu ya Tano na kuanzisha mipya kwa dhamira ya kuwaletea wananchi wote maendeleo endelevu.

Ameyasema hayo leo Juni 8, 2022 akiwa njia kuelekea mkaoni Kagera wakati akiwasalimia maelefu ya wananchi waliojitokeza kumlaki katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Geita na Kagera.

"Awamu iliyopita iliyoongozwa na Kaka yangu Rais, Hayati Dkt. John Pombe nilikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alinifundisha mambo mengi sana na niliisoma dhamira yake vizuri sana kuhusu jinsi ya kuendesha nchi, nataka niwahakikishie dhamira ile tunakwenda nayo na hakuna mradi hata mmoja tuliouanza huko nyuma ambao utakufa na miradi yote mipya itakamilika", alisisitiza Mhe. Rais Samia.

Akieleza zaidi, amesema kuwa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuona wananchi wanapata maendeleo kwa kasi zaidi na huduma bora zinawafikia katika maeneo yao kote nchini.

Baadhi ya miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita ni pamoja na ile ya sekta za maji, elimu, afya, nishati, kilimo, uwezeshaji wananchi kiuchumi, miundombinu katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikilenga kuleta ukombozi wa kiuchumi kwa wananchi wote.

Kwa upande wa Mkoa huo wa Kagera Mhe. Rais amesema kuwa Shilingi bilioni 11 zimeshatolewa kwa ajili ya ujenzi wa Stendi Kuu na kazi hiyo inaendelea ikilenga kuondoa changamoto ya muda mrefu ya ukosefu wa stendi Kuu ya Mkoa wa Kagera mjini Bukoba.

Kwa upande wake Mbunge mstaafu wa jimbo la Muleba, Mhe. Prof. Anna Tibaijuka alimshukuru ,Mhe. Rais kwa kazi nzuri anayofanya katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yuko mkoani Kagera kwa ziara ya siku tatu iliyoanza leo Juni 8, 2022.



# Watanzania Wamekuelewa Mhe. Rais Samia

**Na Ahmed Sagaff - MAELEZO**

Wahenga walinena kuwa ukiona vyaelea ujue vimeundwa na kama vimeundwa ujue waundaji wapo na wana Kiongozi wao katika kuunda hivyo unavyoviona kwa macho yako kila uchao.

Si dhamira yangu kuanza uchambuzi wa kauli hiyo ya wahenga bali ningependa kidogo kueleza hisia zangu kwa kuwa nimeguswa acha niseme, yale yaliyojaa moyoni baada ya kushuhudia umati mkubwa wa Wananchi Waliojitokeza Kumlaki Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia Mhe. Samia Suluhu Hassan leo Juni 8, 2022 katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Geita na Kagera.

Ni wazi kuwa Watanzania wamekuelewa na wanakuunga mkono katika dhamira yako safi ya kuwaletea maendeleo endelevu, tunawapongeza watanzania wote kwa kuonesha umoja na mshikamano usio kifani katika ziara hii, huu ni utamaduni wetu Watanzania tunasifika kwa ukarimu na upendeo ambao leo Rais wetu ameouna kupitia kwa wananchi walaiokusanyika barabarani katika mikoa hiyo.

Ni kwa sababu ya upendo na kazi nzuri anayofanya ya kutekeleza miradi ya maji, barabara, elimu, na afya katika maeneo yote hapa nchini, hii inawapa nguvu watanzania kuendelea kusimama na Serikali yao na kuepuka upotoshaji kwani ukweli wameuona katika maeneo yao, tunajionea Vituo vya Afya, Zahanati na shule zikijengwa kila kona ya nchi hii wala sina haja ya kutaja namba kwa kuwa kila eneo ukifika lina mradi unaoendelea kwa sasa.

Huo ni uzalendo wa dhati, uliooneshwa na Mhe. Rais, Wanakagera mna kila sababu ya kujivunia yale yanayofanyika katika Mkoa wenu, miaka mingi mlikuwa na changamoto ya maji, stendi na kadhalika, sasa Rais Samia kaupiga mwingi neema hiyo mikononi mwenu miradi kibao ya maendeelo inatekelezwa, kazi yenu kushiriki katika utekelezaji na kuilinda.

Nimalizie kwa kusema mimi kama mpita njia nimeguswa na upendo wako kwa Watanzania wote hakika wewe ni Rais wa mfano katika Afrika, KAZI IENDELEE.

Ziara yako Mkoani Kagera itashusha neema zaidi kwa Wananchi wa Kagera na Watanznia kwa ujumla , tuko pamoja nawe katika kueleta maendeleo ya kweli.




2022.MAELEZO PODCASTS.

## MAELEZO PODCASTS

Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts, Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index Podcast Index, AudioMack, Soundcloud

MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ